TANGAZO LA SERIKALI NA. 529 la tareh 28/6/2024

SHERIA YA MISITU
(SURA 323)

# AMRI

*(Imetengenezwa chni ya kifungu cha 29(1))*

AMRI YA KUTANGAZA MABADILIKO YA MPAKA WA MSITU WA HIFADHI TONGOMBA YA MWAKA 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kutangaza Mabadiliko ya Mpaka wa Msitu wa Hifadhi Tongomba ya Mwaka 2024.

Tangazo Ts. Na. 250 la 1961

2. Eneo la ardhi ndani ya mipaka iliyoainishwa katika Tangazo la Msitu wa Hifadhi Tongomba linafanyiwa mabadiliko kusomeka na kuonekana kama lilivyochorwa katika Ramani iliyoainishwa katika Jedwali la Amri hii.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*


WILAYA YA KILWA

MSITU WA HIFADHI TONGOMBA

*Makadirio ya eneo:* Hekta 2058.862 au Kilometa za Mraba 20.589

Unakopatikana na Mipaka

Eneo lote la hifadhi awali chini ya Msitu wa Hifadhi Tongomba unaopatikana katika Wilaya ya Kilwa, Mkoa wa Lindi kama lilivyochorwa katika Ramani ya Idara ya Upimaji Jb 2725 ya mwaka 2017 (Skeli 1:12,500) iliyohifadhiwa na Mkurugenzi wa Idara ya Upimaji na Ramani ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, na lenye mipaka ifuatayo:




Dodoma,
24 Mei, 2024

ANGELLAH JASMINE KAIRUKI,
*Waziri wa Maliasili na Utalii*